



Cour
Pénale
Internationale

International
Criminal
Court

ICC-PIDS-FS-06-008/10_Swa

Ofisi ya Prezidenti na Vyumba



Biro ya Prezida ya Mahakama ya Kimataifa
ya Jinai
Foto: ICC-CPI/Max Koot

Biro ya Prezida na Machumba

Biro ya Prezida, ni moya kati ya bipande ine bya Mahakama. Hii masiku inaundwa na Prezida Sang-Hyun Song (Jamhuri ya Korea), makamu wa kwanza wa prezida Fatoumata Dembele Diarra (Mali) na makamu wa pili wa prezida Hans-Peter Kaul (Ujerumani). Balichaguliwa, siku 11 mwezi ya tatu 2009, kwa kura ya wingi ulio dhahiri ya bajije ba Mahakama juu ya batumike ku Biro ya Prezida muda ya miaka tatu.

Biro ya Prezida iko na kazi ya kuongoza muzuri Mahakama yote, kuacha tu Biro ya Prokirere. Lakini inatumikaka pamoya na Biro ya Prokirere na inaiombaka shauri ku byenye binaangalia mafaa ya bote. Madaraka ya uongozi ya Biro ya Prezida ni sawa vile kusimamia kazi ya Biro ya Grefye tena kufanya kwa ginsi Biro ya Grefye itumikie muzuri Machumba. Kati ya kazi zake za kusimamia, Biro ya Prezida inasaidia ku maneno mingi ya uongozi na inapana njia ya kufuata mu maneno yenye kuangalia uongozi ya Mahakama kwa jumla, sawa vile Kanuni za utumishi, siri ya habari na Mfuko wa Dhamana wa Mahakama.

Mu kazi za Biro ya Prezida muko vile vile kazi za kimahakama na uhusiano na inje. Mukufanya kazi zake za kimahakama, Biro ya Prezida inapangaka kazi ya kimahakama za Machumba na kufanya mapashwa yenye Mkataba wa Roma, Kanuni za Utaratibu na Ushahidi na tena Kanuni za Mahakama zinaomba.

Ndani ya kazi za Biro ya Prezida za uhusiano na inje kuko kutafuta na kufanya makubaliano ku jina ya Mahakama na kufanya kwa ginsi batu bajuwe Mahakama.

Machumba

Sawa vile artikle 39-1 ya Makataba wa Roma inasema, Machumba ziko ndani ya matawi. Zinashurulika na kazi za kimahakama za Mahakama. Kuko matawi tatu : Tawi la utangulizi, Tawi la kesi na Tawi la rufaa.

Kusema tawi jije atatumika ndani inafuata naka na kazi kila jije atatumika na ujuzi na uzoefu ya jije. Hii inafanyika kwa ginsi kila tawi ikuwe na bataalamu ba sheria yenye kuangaliana na maenfraksyo na sheria ya ginsi ya kuongoza masambo yenye kuangaliana na maenfraksyo na sheria ya kimataifa. Bajije benye banatumika ku Tawi la rufaa banafanya kazi mu ile Tawi tu muda yote ya kazi yabo.

Biro ya Prezida inaweza kuamua kuunda machumba zingine za utangulizi wala machumba zingine za kesi, kama uzito ya kazi ya Mahakama inaomba vile, na juu ya uongozi muzuri. Inaweza vile vile kusema jije wa mu Tawi la kesi atumike kwa muda mu Tawi la utangulizi wala wa mu Tawi la utangulizi atumike kwa muda mu Tawi la kesi. Kila tawi inachaguaka prezida wake, yeye njo anaongozaka tawi muda wa mwaka moya.

Tawi la utangulizi

The Pre-Trial Division is composed of judges with Tawi la utangulizi linaundwa na bajije benye banazoweya sana masambo yenye kuangaliana na maenfraksyo. Bajije banatumika muda ya miaka tatu. Hii masiku kuko machumba mbili za utangulizi.

Kila chumba ya utangulizi kiko na bajije tatu, ata kama jije moya anaweza kufanya kazi fulani fulani za ile chumba. Jije prezida wa chumba anachaguliwaka na bajije ba mu ile chumba.